
# Shughuli za Kujifunza Nyumbani



KUJIFUNZA kunafanyika kila pahala, kila wakati na kwa kila mmoja

EENET Enabling Education Network

NAD – The Norwegian Association of Disabled

**EENET – Enabling Education Network**
PO Box 422
Hyde
Cheshire
SK14 9DT
UK

www.eenet.org.uk

info@eenet.org.uk

+44 (0)7929 326 564

This work is licensed under the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License. To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/

# Yaliyomo


**Utangulizi** **4**

**Kubadilisha mazoezi kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum ya kielimu na ulemavu** **6**

**Orodha ya mazoezi (shughuli)** **8–73**

Kitabu cha ABC 8
Jenga mnara 10
Jenga kozi ya kizuizi 11
Kikokotoo 13
Kupika na nambari 16
Buni mchezo wa bao 18
Unaona kile nikionacho mimi 20
Chora mnyama wa 21
Chora mji wako wa kufikiria 23
Vinavyopendwa 25
Elea mashua yako 27
Kwenda sokoni 28
Je! ni maneno managapi? 30
Ningekuwa raisi … 31
Kufanya mahojiano na mtu mzima 33
Vumbua kifaa (chombo au mashine) 35
Mfano wa vitu visivyohitajika 37
Kutengeneza orodha 39
Tengeneza ramani ya eneo lako 40
Tengeneza mtoto bandia kwa soksi 42
Bao au mithili ya mchezo huo 44
Kutazama mazingira 46
Wimbo mpya, sauti/mahadhi ya kale 49
Shairi lisilo na maana 50
Otesha mmea na shuhudia ukikua 53
Kusoma pamoja 55
Msaka vilivyotupwa 58
Fumbo 60
Maumbo na nakshi katika mazingira yetu 62
Mzunguko wa hadithi 64
Kumshukuru shujaa wa kijiji 66
Kusaka Hazina 67
Maswali Ishirini 69
Barua kwa mwalimu wako 71

# Utangulizi

## Mazoezi haya ni kwa ajili ya nani?

- Mazoezi haya ni ya familia zote za watoto wenye ulemavu na wasio na ulemavu.
- Mazoezi haya ni ya kila mtu – mama na baba, walezi, wasichana na wavulana, vijana, ndugu (kaka na dada), babu na bibi, mjomba na shangazi. Kuna fursa nyingi za kujifunza pamoja.

## Haya ni mazoezi gani?

Huu ni 'mkoba wenye mchanganyiko' wa mazoezi ya kufanya nyumbani kwa ajili ya watoto wa kike na watoto wa kiume wa kila rika, walezi na familia. Mtu yeyote anaweza kutumia mawazo yake na ubunifu wake katika kuongezea katika mazoezi haya. Mazoezi mengi yanaweza kufanywa mara nyingi na kwa njia tofauti.

## Kwa nini mazoezi haya yameandaliwa?

Mzoezi haya yanaongeza katika njia nyingi tofauti ambazo watoto hujifunza wakiwa nyumbani. Unaweza kutambua baadhi ya mazoezi haya kwa sababu watoto wako tayari wanafanya baadhi ya mazoezi haya. Yatasaidia familia kuwa na ufahamu zaidi wa namna kujifunza kunavyotokea nyumbani na jinsi kujifunza nyumbani kunavyoweza kusaidia kuimarisha masomo ya shuleni.

## Jinsi ya kutumia mazoezi haya

Angalia mazoezi haya wewe pamoja na mtoto wako. Mwache mtoto wako achague mazoezi ambayo yanamvutia. Mazoezi haya hayahitaji kufanywa kwa mtiririko wowote.

Kuna taarifa inayotolewa kwa kila zoezi, kama ifuatavyo:

> **Utahitaji:** Kisanduku hiki kinaonesha ni matayarisho na vifaa gani vinahitajika katika kufanya zoezi hilo. Mazoezi mengine hayahitaji vifaa, mengine yanahitaji penseli na karatasi, vitu vilivyokwishtumiwa na vitu vyengune vinavyoweza kupatikana karibu na ambavyo havigharimu chochote.
>
> **Mambo ya kufanya:** Maelekezo haya yameandikwa kwa ajili ya mtoto kuweza kufuata. Watoto ambao wanaweza kusoma wanaweza kuzifuata hatua wao wenyewe. Watoto wengine wanaweza kuhitaji msaada wa ziada kutoka kwa kaka/dada au mtu mzima anayeweza kusoma.
>
> **Muendelezo wa zoezi:** Wakati mwengine mazoezi zaidi hujumuishwa ili kuwapa Watoto wakubwa au wenye uwezo zaidi changamoto kubwa zaidi.

Baada ya kila zoezi kuna maelezo ya kukusaidia kuchagua zoezi linalofaa kwa mtoto wako, hii ni pamoja na:

**Umri:** Hii inaonesha ni rika gani linaloweza kuendana, lakini mara nyingi watoto wa kila rika wanaweza kufanya zoezi la aina moja. Kile wanachoweza kufanya kinaweza kutofautiana, kwa mfano watoto wakubwa wanaweza kuandika zaidi, au kuchora kwa uwazi zaidi.

**Msaada wa watu wazima /kaka/ndugu:** Hii inaonesha ikiwa wewe au kaka au dada anaweza kuhitaji kumsaidia mtoto kidogo au sana, au ikiwa anaweza kufanya kazi hiyo peke yake. Maelezo haya yatakusaidia kuamua ikiwa unaweza kuwa karibu lakini ukifanya kitu chengine wakati mtoto wako anafanya kazi hiyo. Wewe au kaka/dada wakati mwengine mnaweza kuhitaji kutoa msaada zaidi kwa watoto wenye mahitaji maalum ya kielimu au ulemavu.

**Utakachojifunza (maarifa) na kile utakachofanya (ujuzi):** Kila zoezi humsaidia mtoto kuongeza maarifa yake, au kufanya mazoezi au kujifunza stadi mpya. Kisanduku kilichopo chini ya kila zoezi kinaonesha ni maarifa na ujuzi gani unaopatikana katika zoezi hilo. Mazoezi mengi yanajumuisha kutengeneza, kujenga au kuunda kitu ambacho kinamsaidia mtoto wako kujizoesha stadi/ujuzi muhimu. Stadi hizi ni pamoja na mawasiliano, kushirikiana (kufanya kazi na wengine), ubunifu, utatuzi wa shida, kufikiri kwa umakini na uratibu wa mwili. Shule na walimu wanajua kuwa stadi hizi ni muhimu. Watoto mara nyingi hawana wakati wa kutosha wa kujizoesha na stadi hizi shuleni. Nyumbani kuna fursa nyingi za kujifunza kupitia kucheza na kupitia kufanya shughuli za kila siku kama kupikia.

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:** Mazoezi mengi hujumuisha maoni ya namna ya kurekebisha au kubadilisha zoezi kwa mtoto mwenye mahitaji maalum ya kielimu au ulemavu. Kazi zote zinaweza kufanywa na watoto wote, lakini watoto wengine wanaweza kuhitaji msaada zaidi au wanaweza kutumia njia tofauti za kufanya shughuli hiyo (kama kuchora au kuzungumza badala ya kuandika; au kulifanya zoezi kuwa rahisi zaidi). Ukurasa unaofuata unatoa maoni zaidi kwa mambo ya kurekebisha. Kwa kuwa wewe ndiye unayemjua mtoto wako vizuri zaidi, basi pia unajua marekebisho yatakayofaa zaidi kwake.

**Kumbuka, kujifunza hufanyika kila mahali, wakati wote.**

# Kubadilisha mazoezi kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum ya kielimu na ulemavu

Kisanduku kilichopo chini ya kila zoezi kinaonesha jinsi ya kubadilisha au kurekebisha zoezi kwa watoto walio na mahitaji maalum ya kielimu na ulemavu. Kila mtoto ni wa kipekee kwa hivyo haya ni maoni ya jumla tu. Mara nyingi mtoto atatuongoza juu ya kile anachokihitaji. Tunapojua watoto vizuri, tunakuwa bora kwa kuwaunga mkono na kujua ni nini wanachokijua, wanachokipenda kufanya na wapi wanahitaji msaada.

Ni sawa kumsaidia mtoto wako, lakini hakikisha huwafanyii mazoezi haya – wanahitaji kuhisi kana kwamba wamefanikiwa kufanya kitu. Usifikirie mtoto hawezi kufanya zoezi hili. Unaweza kupata njia za ubunifu za kurekebisha zoezi ili kila mtu weze kulifanya.

Yafuatayo hapa chini ni maoni zaidi kwa watoto walio na maeneo maalum ya ulemavu au changamoto ya kujifunza. Maoni haya yanaweza kutumika katika mozoezi yoyote.

## Watoto walio na changamoto ya uoni

- **Tumia herufi kubwa:** Ikiwa zoezi linahusisha kuandika, angalia ikiwa mtoto anaona ni rahisi kwake kusoma herufi kubwa au herufi ndogo. Wakati mwengine herufi ndogo ni nzuri kwa watoto , kwa sababu zina 'maumbo' tofauti kwa hivyo ni rahisi kusoma na kuzitambua.
- **Tumia rangi:** Tumia rangi tofauti, ikiwezekana, kuandika maneno ambayo ni msingi katika kujenga sentensi, (kwa mfano, vitenzi vya kawaida kama 'sema' 'leta' na 'toa'). Hii inaweza kufanya kusoma au kuandika kuwa rahisi kwa mtoto.
- **Tumia vifaa vyenye vinavyoweza kuguswa kutengeneza** na kujenga vitu, kwa hivyo watoto ambao wana ugumu wa kuona wanaweza 'kuhisi' na 'kugusa' kile wanachojaribu kukiunda. (Kwa mfano, jenga mnara kwa kutumia vitu vilivyotengenezwa kwa vifaa tofauti.)
- Kumbuka, maoni haya yanaweza kusaidia watoto wote pia, sio wale ambao wana ugumu wa kuona tu.

## Watoto wenye changamota ya usikvu

- **Tumia lugha ya alama** ikiwa wewe na mtoto wako mnaijua. Au jifunze maneno kadhaa ya msingi ya lugha ya alama pamoja na mtoto wako.
- **Muelekee uso kwa uso mtoto** ambaye hawezi kusikia vizuri na useme kwa ufasaha (usipige kelele). Tumia l**ugha ya mwili, ishara za uso na ishara za mikono** kusaidia maana ya kile unachokiwasilisha.

- Jaribu kufanya mazoezi haya katika sehemu zenye taa nzuri, ili mtoto akuone na aweze kusoma kwa kuangalia midomo yako. Zungumza kwa kasi ya kawaida na usimung'unye maneno.
- Tumia penseli na karatasi (au chaki na ubao) wakati wa kufanya mazoezi haya kwa ajii ya kuandikia vitu, au chora picha kusaidia kuelezea kitu.
- Kumbuka, baadhi ya maoni haya yanaweza kusaidia watoto wote pia, sio wale tu ambao wana chanagamoto ya kusikia.

## Watoto ambao wana changamoto ya kutembea

- Weka nyenzo na vifaa karibu: Hakikisha vitu unavyovihitaji kwa ajili ya zoezi lako huhifadhiwa pahala ambapo mtoto anaweza kupafikia.
- Jaribu kutumia vitu kwa saizi zinazosaidia watoto katika stadi za uratibu. (Kwa mfano, penseli kubwa na kalamu zinaweza kuwa rahisi kushikilia.)
- Mwongozo na vitendo vya msaada vilikuwa muhimu, (kwa mfano, unaweza kuhitaji kusaidia kumsogezea kete zinazozunguka wakati wa mchezo wa bao.)
- **Punguza nafasi:** Badilisha mazoezi ili yafanyike katika nafasi ndogo, kwa kutumia harakati kidogo, (kwa mfano, kutafuta au shughuli za kusaka hazina zinaweza kufanywa katika chumba kimoja badala ya nyumba nzima au eneo la nje.)

## Watoto wenye uzito wa kujifunza


- **Rahisisha zoezi** kwa kufanya sehemu tu . (Kwa mfano, imba beti moja ya nyimbo ya 'New song, old tune', na sio beti tatu; andika orodha fupi katika –'Kuandaa orodha'. Mtoto wako anaweza pia kuandika neno moja moja badala ya sentensi nzima ili kuwasilisha mawazo yake.
- **Chora badala ya kuandika.** Mazoezi mengi tayari yanajumuisha kazi za kuchora. Kwa mazoezi ambayo yanamtaka mtoto kuandika, anaweza kuwasilisha maoni yake kwa njia ya kuchora badala ya kuandika.
- Yagawe maelekezo katika hatua rahisi na muombe mtoto afanye moja tu kwa wakati. (Kwa mfano, 1) kwanza pokea penseli na karatasi, 2) kisha uchore umbo, 3) kisha upake rangi, 4) umalizie kwa kuweka alama.)
- Rudia maelekezo mara mbili au tatu ili mtoto aweze kukuelewa na kufahamu maelekezo.

Kila mara wacha watoto wakuongoze. Watakujulisha ikiwa wanaelewa, na wanavutiwa na kufanya zoezi hilo au la. Toa msaada kwa upole na usiweke shinikizo kwa watoto. Mara nyingi husaidia kukiri zoezi ni gumu na kisha kulibadilisha kuwa zoezi la pamoja. Unaweza kusema "Hiyo ni ngumu sana, au siyo? Je! Tujaribu kuifanya pamoja?"

# Kitabu cha ABC

**Utahitaji:** Penseli za rangi, karatasi, gundi or sindano na uzi

## Mambo ya kufanya:




- Andaa karatasi na penseli za rangi.
- Kunja vipande vya karatasi ili kufanya kitabu cha alfabeti. Utahitaji karatasi ngapi?
- Panga jinsi utakavyoziandika hizo herufi. Moja kwenye kila ukurasa? Mbili? Pamoja na picha za vitu / wanyama ambao majina yao yanaanza na herufi hiyo?
- Buni na chora ukurasa wa juu wa kitabu chako. Kumbuka kuweka jina lako kama 'mwandishi' (mwandishi wa kitabu hicho).
- Fikiria jinsi ya kuziandika hizo herufi za alfabeti. Je! herufi zitaonekana kama vikatuni au zitaonekana kama kamba? Zipake rangi kama unazo.
- Ongeza maneno ambayo yanaanza na herufi hiyo ya alfabeti kwenye kila ukurasa.
- Kikunje kitabu chako na muombe mtu mzima akushonee kitabu chako kwa uzi na sindano au akibandike gundi ili kikae pamoja.

### Muendelezo wa zoezi

- Soma kwa sauti au muombe mtu akusomee hadithi hii

### Machafuko katika ardhi ya Alfabeti

Siku moja mapacha 'e' na 'e' waliamua kufanya burudani. Kwa hivyo waliingia katikati ya maneno yote ambayo wangeweza kuyafikiria. Waligeuza 'ship' kuwa 'sheep' na kondoo walirowa maji sana na kuchanganyikiwa. Waligeuza 'chick' kuwa 'cheek' na mama kuku alitumia siku nzima kumtafuta mtoto wake. Waligeuza 'stir' kuwa 'steer' na mpishi hakujua alichokuwa akifanya. Walimgeuza Will kuwa wheel na akabiringitia kuteremka kilima. Mapacha walicheka sana. Lakini herufi nyengine za alfabeti hazikuona kuwa hicho kuwa ni kitu cha kuchekesha. Hatimaye, mkuu wa herufi alisema, 'Sawa sasa basi inatosha. " Kisha akawaweka mapacha katikati ya 'slip' na kuwafanya waende zao kulala.

- Je! Unaweza kutengeneza hadithi yako mwenyewe kuhusu machafuko katika ardhi ya alfabeti?

**Umri:** Msingi

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Wastani

**Utakachojifunza:** Herufi za alfabeti, kukuza lugha, msamiati, tahajia

**Utakachokifanya:** Ubunifu, uratibu, usanifu

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:**

- Buni nyimbo kuhusu alfabeti
- Muombe mtu mwengine akusaidie kutengeneza kitabu
- Tumia vijiwe vidogo au vifuniko vya chupa kutengeneza alfabeti juu ya meza au sakafu

# Jenga mnara

**Utahitaji:** Ubao wenye kadi au vifungashio vya plastiki, visanduku vidogo, mawe yaliyonyooka

## Mambo ya kufanya:

- Kusanya vitu vingi visivyo na mwinuko chini. Hii inaweza kujumuisha visanduku vya zamani, katuni zilizo na vifuniko, vitabu, mawe madogo yasiyo na ncha, mitungi ya plastiki iliyo na vifuniko....
- Jaribu kujenga mnara kwa kutumia vitu hivyo. Je! Unaona nini kuhu kitu unachoweza kuweka juu ya kingine? Je! Vitu vipi vikubwa? Ikiwa utaweka kitu kidogo chini ya mnara wako, nini kinatokea?
- Je! Unaweza kujenga mnara wako kwa urefu gani? Ni nini hufanya mnara wako kusimama au kuanguka? Unawezaje kuufanya uwe na nguvu?



**Umri:** Msingi

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Mizani, muundo

**Utakachokifanya:** Majaribio, ubunifu, uratibu na ufahamu wa anga

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:**

- Mwombe mtu mwengine akusaidie kujenga mnara wako.
- Ikiwa unapata ugumu wa kuona tumia vitu unavyoweza kuvigusa na uweze kuhisi 'mnara'.

# Jenga kozi ya kizizi

**Utahitaji:** Samani, vitu vikubwa kama vile maboksi au vipande vya mbao, matairi makongwe n.k.

## Mambo ya kufanya:

- Kozi ya kizuizi ni seti ya vizuizi ambavyo unahitaji kuvipanda juu, kupita chini yake au katikati. Inaweza kujumuisha kukimbia, kuruka, kutambaa, kupanda na kuweka uwiano. Unaweza kuifanya iwe rahisi au ngumu kadiri unavyopenda. Tazama mfano kwenye picha.

- Tafuta nafasi (ndani au nje) ambapo unaweza kuunda kozi ya kizuizi. Kusanya vitu kadhaa kwa ajili kizuizi hicho: kwa mfano, vipande vya mbao, mawe makubwa ya kukanyaga ili mtu aweze kupita, matairi makongwe, samani mbalimbali za zamani. Mshirikishe mtu mzima katika kuhakikisha iwapo ni sawa kuvitumia vitu hivyo.



- Buni na jenga kozi yako ya kizuizi. Fikiria ni nani atakayekitumia kizuizi hicho. Fanya iwe changamoto kwao lakini usiifanye kuwa isiyowezekana!

- Kijaribu kizuizi chako- je, kuna kitu ungependa kubadilisha? Mwombe mtu akutizamie muda wakati unakizunguka kizuizi chako. Unaweza kukizunguka kwa muda gani? Unaweza kukizunguka kwa muda gani?



**Umri:** Msingi

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Wastani

**Utakachojifunza:** Ubunifu, ujenzi

**Utakachokifanya:** Ubunifu, utatuzi wa shida, uratibu, uhamasishaji wa anga


**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:** Ifanye kozi yako ya kizuizi kuwa ni rahihi kwa mtu ambaye anapata ugumu wa kutembea au ambaye anapata ugumu kuona. Hakikisha unajumuisha harakati anazoweza kufanya, kama kugonga, kutambaa na / au vitu anavyweza kuvigusa vyenye ili aweze 'kuvihisi' wakati akizungukazunguka katika njia n.k.

# Kikokotoo

**Utahitaji:** Penseli/peni na karatasi Chaki

## Mambo ya kufanya:


- Nakili mchoro huo kwenye karatasi, au tafuta eneo kubwa ardhini ambalo unaweza kuchora kwa chaki.





- Mchezo huu unahusu kucheza na nambari. Kutoka 'ANZA' unapita kwenye mistari hadi katika 'MALIZA'. Unaweza kwenda katika mstari ulionyooka au zig-zaga au mstari (njia) yoyote nyengine.

- Kadiri unavyopita kwenye mistari unafanya hesabu (jumla) ukitumia nambari unazopita ili kuishia na nambari ya mwisho kwenye MALIZA.


- Ni njia ngapi tofauti unazoweza kuzipata ambazo ukuzijumlisha zitafikisha namba 8?




**1.**
2 x 4 = 8




**2.**
2 + 2 + 4 = 8




**3.**
3 x 4 − 4 = 8
(12) − 4 = 8

Jawabu: kuna njia tatu zinazoweza kufanya hivyo

- Kanuni ni:
  - Kila njia lazima iwe tofauti
  - Hakuna njia inayoweza kupitia nambari kwa zaidi ya mara moja.
  - Kila wakati unapoipita nambari lazima uitumie kuongeza, kutoa na / au kuzidisha ili ujumuishe nambari hiyo katika hesabu yako.

- Je! Unaweza kupata njia ambayo itasababisha kupatikana nambari 10? Je! Ni vipi kuhusu njia mbili ambazo zitasababisha kupatikana kwa nambari 16? Andika mahesabu yako.

- Je! Ni njia zipi nyengine na nambari za mwisho unazoweza kubuni? Je ni nambari ipi kubwa zaidi unaweza kuifanya? Je! ni nambari ipi ndogo zaidi unayoweza kutengeneza? Je! ni idadi gani ya nambari za mwisho unazoweza kutengeneza kwa pamoja?

**Muendelezo wa zoezi:**

- Mpe mtu mwengine nambari ya mwisho na mwombe atafute njia nyengine. Anaweza kupata njia ambazo hukuzifikiria!

- Badilisha nambari zilizo kwenye mchoro na nambari zako mwenyewe. Nambari zozote zinawezekana lakini ni bora kuweka nambari za mlango wa mamoja au mlango wa makumi.

- Unaweza kutumia nambari zenye decimali ili kuzifanya ziwe zenye changamoto zaidi. Kwa mfano, 0.5 x 4 = 2 au 2,5 x 5 = 12.5.

**Umri:** Wowote

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Wastani

**Utakachojifunza:** Kukokotoa mahesabu, kujumlisha, kutoa na kuzidisha

**Utakachokifanya:** Utatuzi wa matatizo, kufikiri kwa umakini, ushirikiano, mawasiliano

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:** Chora mchoro mkubwa kwenye sakafu kwa kutumia chaki na 'pita' katika njia zake na utakusaidia ukumbuke mahesabu vizuri zaidi. Weka nambari zisizozidi 1-5 katika mchoro huo.

# Kupika na nambari

**Utahitaji:** Penseli au kalamu na karatasi Vitu vya kupika Vyombo vya kupikia

## Mambo ya kufanya:

- Amua ni kitu gani ungependa kupika. Panga chakula chako na mtu mzima au ndugu iwapo utahitaji msaada.
- Andika orodha ya vitu vitu utakavyovihitaji katika kupika.
- Amua ni watu wangapi utakaowapikia chakula hicho. Ni kiasi gani ya kila kitu kitakachohitajika kwa idadi hiyo ya watu? Andika idadi au kiwango cha kila kitu kitakachohitajika katika orodha .
- Je itakuwa ni idadi au kiwango gani iwapo ungetakiwa kuwapikia wat umara mbili Zaidi ya hao? Nusu ya hao? Wawili zaidi?
- Weka tayari mahitaji vyako pamoja na vyombo vya kupikia (vyungu au vyuma vya kupikia).
- Jadili hatua / maelekezo ya mapishi yako na andika kila hatua. Tumia maneno ya kuelezea upishi kama vile 'katakata', 'menya', 'koroga' na 'changanya'.
- Fuata kila hatua ya mapishi na urekebishe maagizo yako ya maandishi kadiri unapoendelea na upishi, jaribu kuwa wazi iwezekanavyo ili mtu mwengine aweze kufuata mapishi yako.
- Mara umalizapo kupika waite wanafamilia kuja kula ulichopika.
- Fikiria namna ya kugawa sawasawa ulichokipika kwa mujibu wa idadi ya watu waliopo. Je, kila mmoja atapata vijiko, slesi/vipande vingapi? Je, kuna chakula cha kutosha kwa wanaotaka kuongeza?

## Muendelezo wa zoezi:

- Andika mapishi yako vizuri ili mtu mwengine aweze kufuata maagizo. Waombe wapike kwa kufuata maandishi yako kisha wakupe maoni (kukuambia) kwa kiasi gani maelekezo yalivyokuwa wazi na ikiwa mabadiliko yoyote yanapaswa kufanywa.



- Chagua mapishi ambayo unaweza kukigawa chakula utakachopika katika vipande, kama keki au biskuti au kukata matunda ili kufanya saladi ya matunda. Tengeneza vipande tofauti na uviandike (kama ilivyo katika picha hapo juu).
- Tengeneza 'kitabu cha mapishi' chenye mapishi yako yote unayopenda.

**Umri:** Wowote

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Wastani / juu

**Utakachojifunza:** Hesabu, kutumia hesabu, kupima, kupanga mapishi, ukuzaji wa lugha

**Utakachokifanya:** Ubunifu, mawasiliano, utatuzi wa shida, kufikiri kwa umakini muhimu, uratibu

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:**

- Mwombe mtu mwengine akusaidie kupika.
- Toa maelekezo kwa mdomo badala ya kuyaandika
- Mwombe mtu mwengine ayaandike maelekezo hayo
- Chora picha kwa kila hatua ya mapishi


# Buni mchezo wa bao

**Utahitaji:** Penseli za rangi au kalamu, karatasi kubwa, vitu vidogo vidogo, mikasi, kete au kete za karatasi zilizotengenzewa nyumbani

## Mambo ya kufanya:

- Weka tayari karatasi na penseli, rangi tofauti ikiwa inawezekana. Weka karatasi kubwa wazi kwenye meza au kwenye sakafu.

- Chora visanduku  kadhaa vyenye umbo la mraba vilivyounganishwa kwenye karatasi ili kutengeneza 'njia' kwenye  karatasi, (tazama picha hapa chini). Onesha wazi wazi sehemu ya kuanzia na kumalizia.




- Acha visanduku vingi kwenye bao la mchezo huo kuwa wazi. Kwenye nafasi nyengine andika 'pata kadi'. Ongeza nafasi chache ambazo zinaelekeza wachezaji mbele au nyuma, kwa mfano, 'rudi nyuma nafasi 2', 'umekosa '…. Unataka mchezo kuwa na ugumu wa kutosha kuufanya  kuwa wa kuvutia, lakini usiufanye kuwa mgumu sana na kuwa haiwezekani kushinda.

- Kata karatasi katika maumbo madogo madogo ya mraba. Upande mmoja wa kila mraba mdogo andika maelekezo / shughuli. Kuwa mbunifu na jaribu kuwa na mchanganyiko wa maelekezo ya aina tofauti! Kwa mfano:

  - Ukweli kuhusu hisabati: hesabu katika 3, 6, 8 ...
  - Vitendo vya mwili: zunguka mara tatu, gusa kichwa chako na usugue tumbo lako wakati unapohesabu hadi 20,
  - Unda orodha ya maneno ambayo yana vina sawasawa
  - Imba nyimbo
  - Ujuzi wa jumla: Taja miji mikuu mitano (5) ...

- Wewe pamoja na wachezaji wengine kubalianeni kuhusu kanuni kadhaa za kucheza, ni nani anayepaswa kuanza? Ni nini kinatokea ikiwa mtu hawezi kufanya shughuli? Unaweza kuomba msaada? Je! Unaweza kupitisha zamu? Baada ya kukubaliana na kanuni hizo ni wakati wa kuanza kucheza.

- Weka kadi za 'shughuli' karibu na bao la mchezo. Kila mchezaji achague kitu kidogo cha kuzunguka kwenye bao. Kila mchezaji achukue na kuzungusha kete wakati wa zamu yake.

- Wakati mchezaji anatua kwenye 'kupata kadi', chukua kadi ya shughuli. Fanya kazi hiyo iliyoandikwa kwenye kadi. Ikiwa mchezaji hawezi, rejelea kanuni zilizokubaliwa awali.

- Mchezaji wa kwanza anayemaliza hadi mwisho ndiye atakayekuwa mshindi.

**Umri:** 8+

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Wastani

**Utakachojifunza:** Kukuza lugha, kutumia nambari, maarifa ya jumla

**Utakachokifanya:** Mawasiliano, mashirikiano, kufikiri kwa umakini

# Unaona kile nikionacho mimi

**Utahitaji:** Karatasi na penseli/kalamu

**Mambo ya kufanya:**

- Chora picha.
- Kisha, andika maelekezo ya namna yakuchora pich hiyo.
- Mwombe mtu mwengine afuate maelekezo yako bila ya kuona mchoro wako.
- Akishamaliza, ilinganishe michoro hiyo. Unaonaje? Je, ni sawasawa au tofauti? Kwanini zinatofautiana? Kitu gani kingifanya iwe sawasawa?



**Umri:** Wowote

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Ukuaji wa lugha; maelekezo ya maandishi


**Utakachokifanya:** Ubunifu, uratibu; mawasiliano

# Chora mnyama wa ajabu

**Utahitaji:** Penseli na karatasi

## Mambo ya kufanya:

- Weka karatasi na penseli tayari, zenye rangi tofauti tofauti.
- Fikiria paka mwenye mkonge kama tembo? Au mbwa mwenye na magamba? Je! Hiyo ingeonekanaje?
- Chora mnyama wako wa ajabu aliye na sehemu tofauti za wanyama wengine. Weka alama kwa kila sehemu tofauti za wanyama.
- Mpe jina mnyama wako wa ajabu. Jina linaweza kuwa kidokezo kwa wanyama tofauti ambao umetumia katika mchoro wako.




## Muendelezo wa zoezi:

- **Fikiria:** Anaishi wapi (katika ulimwengu wetu au mwengine? ulimwengu wa aina gani?), Anakula nini, sauti yake ikoje, anatembeaje? Alipataje sehemu zake tofauti za wanyama?
- **Simulia / andika hadithi** kuhusu mnyama huyo.
- **Soma hadithi ifuatayo** (au mwombe mtu mwengine akusomee)

### Fisi na Sungura

Fisi alikuwa akiuza mbogamboga sokoni na kila wakati Sungura alikuwa akimdhihaki. Huwezi kukimbia haraka kama niwezavyo mimi, au unaweza? Alimkebehi. 'Wewe ni mzee na huwezi kuona vizuri.' Sungura alikimbia huku akicheka. 'Nitamwonyesha' siku moja, alisema fisi. Kwa hivyo, alijifanya kuwa haoni vizuri, na alivaa miwani myeusi. Sungura aliibuka na ujasiri, na akamkaribia zaidi. Na kisha, siku moja, Fisi akakunjua miguu yake na kumshika Sungura kwa masikio.

Hakumuachia kwenda popote. Alijifanya kumla sungura kwa masikio yake. Sungura alijikurupusha na kujitikisa lakini Fisi aliendelea kumning'iniza sungura juu na chini kwa masikio yake ambayo yalianza kuwa marefu na kuendelea kurefuka hadi mwishowe Sungura akaweza kujinasua na kuwa huru kutoka katika makucha na taya za fisi (meno ya fisi bado hayakuwa mazuri sana) na akatimua mbio haraka sana akaenda mbali na soko, na mji, na kuwa mbali na fisi. Ndio maana unaona, hadi leo sungura wana masikio marefu.

**Umri:** Msingi

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Maumbo na rangi; lugha ya kuelezea

**Utakachokifanya:** Ubunifu, uratibu

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:**

- Fafanua kuhusu mnyama. Mwelekeze mtu mwengine kumchora mnyama huyo.
- Tumia udongo au chupa zilizotumiwa na vifungashio vya chakula kutengeneza mnyama.

# Chora mji wako wa kufikiria

**Utahitaji:** Karatasi na penseli/penseli za rangi

**Mambo ya kufanya:**

- Tayarisha karatasi kubwa na penseli.
- Muombe mtu akusomee kwa sauti matini ifuatayo pole pole ili uweze kufumba macho yako na kufikiria.

  Fumba macho yako na ufikirie kuhusu mji wako. Chukulia kuwa unatembea kwenye barabara ya mji wako wa kufikiria. Mji wako unaonekanaje? una majengo gani? Majengo yake ni marefu? Kuna aina gani ya usafiri? Kuna kituo cha reli? Ni mji wa 'kijani kibichi' wenye miti na mbuga? Au ni mji wa kisasa wenye teknolojia ya juu na magari yanayoruka? Chukua dakika chache kufikiria mji wako huo.

- Fungua macho yako. Chora mji wako. Panga phala yatakapokaa majengo na vitu vyengine. Fanya makisio kwanza kisha ujaze sehemu iliyobaki. Tumia rangi ikiwa unayo.
- Utaupa jina gani mji wako?
- Angalia mji wako tena. Je! Umesahau chochote? Mahali pa kusalia? Ngome ya zamani au jumba la kumbukumbu? Je! vipi kuhusu mto na mahali pa kucheza? Je! Watu wanaweza kutembea kwa urahisi katika mji? Vipi kuhusu watu wenye ulemavu? Fanya mji wako uwe mkubwa ili kuongeza vitu hivi




**Umri:** Msingi

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Wastani

**Utakachojifunza:** Kukuza lugha, mizani, jinsi miji inavyofanya kazi

**Utakachokifanya:** Ubunifu, kupanga, kusanifu, utatuzi wa shida

# Vinavyopendwa

**Utahitaji:** Penseli au kalamu na karatasi na rangi tofauti

## Mambo ya kufanya:

- Chora mkono wako katikati ya kipande cha karatasi.
- Kwenye mchoro, ndani ya kidole gumba andika rangi unayoipenda.
- Kwenye vidole vyako vyote vilivyobaki, andika somo unalolipenda skuli, chakula unachokipenda, mchezo unaoupenda, na mnyama unayempenda.
- Nafasi iliyobakia ipambe kwa picha za vitu unavyovipenda!



### Muendelezo wa zoezi:

- Tengeneza vitu tofauti vya kuandika kwenye vidole vyako, hivi vinaweza kuwa vipengele vyengine unavyovipenda au aina tofauti za maneno kama vile mji mkuu, samani ndani ya nyumba yako, vitu unavyovipenda kufanya na kadhalika.



**Umri:** Msingi

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Kukuza lugha

**Utakachokifanya:** Ubunifu, uratibu

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:**

- Mwombe mtu mwengine akuchoree ulipoweka mkono wako.
- Mtajie mtu vitu unavyovipenda zaidi.
- Fikiria vitu vyengine unavyovipenda.

# Elea mashua yako

**Utahitaji:** Vibomba vya plastiki vilichotumika au vya chupa vipande vya karatasi au kitambaa au vijiwe

## Mambo ya kufanya:

- Tafuta vipande vikongwe vya plastiki au chupa za plastiki.
- Buni mashua yako, je! Utaongeza meli?
- Iweke mashua yako katika ndoo ya maji au bwawa dogo; Inakuaje? Je! Unaweza kuifanya ivuke kwenye maji?
- Kusanya vijiwe kadhaa. Je! Itachukuwa vijiwe vingapi kable ya kuzama?





**Muendelezo wa zoezi:** Je! Unaweza kutengeneza mashua kwa kutumia vifaa tofauti? Chukuwa mfano wa karatasi? Je! Hii inaweza kubadilisha na kuchukuwa vijiwe vingapi?

**Umri:** Msingi

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo / wastani

**Utakachojifunza:** Sayansi (fizikia); tungamo (wiani)

**Utakachokifanya:** Ubunifu, uratibu, usanifu

# Kwenda sokoni

**Utahitaji:** Vifaa vya 'kuuza' katika soko lako, penseli na karatasi

## Mambo ya kufanya:

- Tafuta nafasi ya kuanzisha duka lako katika soko. Inaweza kuwa meza ndogo au nafasi tu kwenye sakafu mahali pengine.
- Amua utauza nini katika duka lako. Chakula? Nguo? Vitabu? Au mchanganyiko wa vitu?
- Kusanya vitu kwa ajili ya duka lako. Muulize mtu mzima au ndugu mkubwa ikiwa ni sawa 'kukopa' vitu kwanza. Unaweza kutumia pia vijiwe, vifungo, vifuniko vya chupa, majani, vijiti kama vitu vya 'kuigiza' kuuza.
- Tumia vijiwe au vifuniko vya chupa kama pesa za 'kuigiza'. Tafuta kisanduku kidogo cha kuwekea pesa. Weka karatasi na penseli tayari ili ujue cha kutoa.
- Weka duka lako. Panga vitu vyako vizuri. Andika bei kwenye vipande vya karatasi na uziweke karibu na bidhaa kwenye duka yako.
- Fungua duka lako na uwaalike wateja waje.
- Lifanye duka lako lipendeze na si lazima kuweka vitu ambavyo wateja wako wanataka. Weka vitu vingine badala yake. Au weka bei ya juu na uwape sababu. Je! Wataikubali bai ya juu?




**Umri:** Msingi

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Wastani

**Utakachojifunza:** kujumlisha na kutoa na kukokotoa gharama ya punguzo, lugha ya kununua na kuuza

**What you wil practice:** Mawasiliano, mazungumzo, kushirikiana, ubunifu, utatuzi wa shida

# Je! ni maneno managapi?

**Utahitaji:** Penseli au kalamu na karatasi

## Mambo ya kufanya:

- Andika senstensi 'Kujifunza nyumbani ni raha'.
- Angalia ni maneno mangapi tofauti unaweza kuyafanya kautoka katika sentensi na ufanye orodha, kwa mfano: nyumba, funza, uji, umba.
- Jee unaweza kutunga sentensi mpya kutoka orodha ya maneno hayo?
- Fikiria sentensi tofauti na uwaulize watu wengine ni maneno mangapi wanaweza kuyafanya.
- Angalia sentensi iliyo chini ambayo hutumia kila herufi katika alfabeti: 'The quick brown fox jumps over the lazy dog.'
- Ce! Unaweza kutunga sentensi inayotumia herufi za alfabeti ambazo hazitumiwi sana? Kama vile q au x? Je! Unaweza kutumia maneno mangapi tofauti kutoka sentensi yako mpya?

## Muendelezo wa zoezi:

- Tengeneza mchezo wa neno kwa kutumia maneno.
- Tengeneza hadithi fupi ukitumia maneno mapya na uiandike chini.

**Umri:** Wowote

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Makuzi ya lugha; kuandika, tahajia, muundo wa sentensi

**Utakachokifanya:** Mpangilio, upangaji, ubunifu

# Ningekuwa raisi ...

**Utahitaji:** Karatasi na penseli/kalamu

## Mambo ya kufanya:

- Fikiria wewe ni rais wa nchi yako. Je! ni kitu gani cha kwanza utakachokibadilisha? Je ungependa kufanya nini juu ya yafuatayo:
  - Elimu (kwa mfano, skuli na walimu)
  - Mazingira (kwa mfano, kuhifadhi maumbile)
  - Huduma ya afya (kwa mfano, hospitali, madaktari na wauguzi
  - Usafiri (kwa mfano, jinsi watu wanavyoweza kutembea sehemu mbalimbali)
- Je! Kuna vikundi vya watu ungependa kuvisaidia? Ni akina nani? Je! Ungewasaidiaje?
- Nakili jedwali na ukamilishe sentensi kwa kutumia maneno yako mwenyewe.
- Ongeza sentensi nyingi zaidi kama unavyohitaji.
- Fanya iwe hotuba ya 'Raisi' kwa kusoma sentensi zako kwa sauti na kwa kujiamini.



## Ningekuwa raisi (jina lako)

Ningekuwa raisi wa (nchi yako), Ningeli……………………………
…………………………… na kisha ningeli ……………………………
Kungekuwa na ……………………………
Ningelifuta ……………………………
Kusingekuwa tena na ……………………………
Ningehakikisha kwamba ……………………………

Saini: ________________________

**Umri:** Wowote

**Utahitaji:** Pencil or pen and paper

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Makuzi ya lugha; sarufi ( Shuruti ya 2)

**What you wil practice:** Ubunifu, kufikiri kwa makini, mawasiliano, kuzumgumza katika hadhara

# Kufanya mahojiano na mtu mzima

**Utahitaji:** Karatasi na penseli/kalamu

## Mambo ya kufanya:

- Fikiria mtu mzima mwenye mvuto ambaye angependa kuhojiwa. Inaweza kuwa ni mtu yeyote katika familia yako au katika jamii yako.
- Ni nini kinachomfanya awe na mvuto? Unataka kumuuliza nini? Kuhusu wakati wake wa utoto? Mabadiliko aliyoyaona? Uzoefu maalum?
- Andika mambo unayotaka kumuuliza. Angalia maswali yako na uweke nambari kwa mpangilio ambao ungependa kuyauliza.
- Fanya mahojiano ya 'mazoezi' na mtu mzima mwengine au kaka/dada yako. Hii itakusaidia kuona ikiwa unahitaji kubadilisha chochote. Je! Mhojiwa alikuona wewe kuwa ni mpole? Mkali sana? Je! alitaka wakati zaidi wa kukuelezea mambo uliyoyataka?
- Fanya mabadiliko yoyote ambayo unafikiria unahitaji baada ya mazoezi yako. Je! Unahitaji maswali zaidi? Machache? Je! Unataka kubadilisha maswali yoyote?
- Fanya mahojiano. Mshukuru mhojiwa kwa kutumia muda wake pamoja nawe.

## Muendelezo wa zoezi:

- Andika maswali ya mahojiano kama maandishi yatakayotangazwa kwenye redio na/au makala katika gazeti litolewalo katika eneo unaloishi.




**Umri:** 8+

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Kukuza lugha; kujifunza kuhusu familia au historia ya jamii

**What you wil practice:** Mawasiliano, kuandaa na kupanga mahjiano, kufikiri kwa umakini

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:**

- Muombe mtu akuhoji wewe kwanza ili upate kujua nini cha kuuliza
- Andika maswali ya mahojiano kwa hati kubwa ili yawe rahisi kuyaona.
- Fanya maswali hayo kuwa mafupi ili iwe rahisi kuyakumbuka
- Muombe mhojiwa akupe majibu katika sentensi fupifupi ili iwe rahisi kwako kuyaandika

# Vumbua kifaa (chombo au mashine)

**Utahitaji:** Penseli au peni na karatasi

## Mambo ya kufanya:

- Fikiria juu ya kifaa (zana au mashine) unayotaka kuvumbua. Kinafanya nini? Labda ni kitu ambacho kinaweza kusaidia watu? Je! Unaweza kinaweza kutumia kwa kusafiria? Kimetengenezwa kwa kitu gani ? Kinatumia umeme?


- Chora picha ya kifaa chako na uwekeze lebo. Je! sehemu zake mbalimbali ni zipi?

- Andika juu ya kifaa chako. Unaweza kuelezea jinsi kinavyofanya kazi? Je! Unaweza kufanya nini kwa kutumia kifaa chako?

## Muendelezo wa zoezi:

- Fanya kifaa chako kwa kutumia vitu vilivyokwishatumika. Kwa mfano, tafuta maboksi yaliyotumiwa na chupa za plastiki. Ukipenda, andika kwenye sehemu tofauti za kifaa chako.

- Andaa tangazo la kifaa chako. kitauzwa pahala gani? Je! kifaa chako kinafanya jambo gani ambalo litafanya watu 'kukinunua'? Je! kitafanya vipi maisha ya watu kuwa bora? Kinagharimu kiasi gani? Andika tangazo lako katika gazeti linalotolewa katika eneo lako.



**Umri:** Msingi

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Usanifu, makanika (ufundi), kutengeneza vitu

**Utakachokifanya:** Ubunifu, utatuzi wa changamoto, uratibu, uwelewa wa anga

# Mfano wa vitu visivyohitajika

**Utahitaji:** Pencil or pen and paper, penseli au kalamu na karatasi

## Mambo ya kufanya:

- Kusanya vitu vilivyotengenezwa kwa kutumia vitu vilivyotumika na vifungashio. Hii inaweza kujumuisha chupa za plastiki zilizotumiwa, vifuniko vya chupa, maboksi ya ukubwa wa saizi zote, katuni, vifungo vya zamani vya nguo na kadhalika.
- Pia tafuta bidhaa asilia ambazo unaweza kuzitumia kwa Mfano wa Vitu visivyohitajika, kwa mfano vijiti, vijiwe, majani makavu, au hata udongo au hata matope.





- Fikiria namna utakavyopenda kufanya. Mdoli? Je! Una matairi? Au pango? Na kuta? Fikiria juu ya muundo wa kile unachotaka kukitengeneza.

Hizi ni kama mifano:

- Chora picha ya muundo wako na panga ni nini unahitaji kukifanya.
- Tengeneza mfano wako.
- Angalia mfano wako tena. vipi utaweza kufanya vizuri zaidi? Ni nini kingesaidia kuiimarisha? isaidie iende vizuri?



**Umri:** Msingi

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Design, mechanics, construction

**Utakachokifanya:** Creativity, problem-solving, coordination, spatial awareness

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:**


- Muombe mtu akusaidie kutengeneza mfano wako.
- Toa maelekezo kwa maneno / Sema maelekezo? kwa kutengeneza mfano wako na muombe mtu mwingine akufanyie wewe?
- Weka muundo rahisi - tengeneza sufuria kwa mmea, kitu ambacho unaendelea, mchezo wa kuhesabu.

# Kutengeneza orodha

**Utahitaji:** Penseli au kalamu na karatasi

**Mambo ya kufanya:**

- Fikiria mambo kadhaa ambayo unaweza kuyetengenezea orodha:
  - nyimbo unazozipenda
  - mimea katika eneo lako
  - vitu vinavyokufanya ufurahi
  - vitu amabvyo unaweza vizuri kuvifanya vizuri
  - vitu unavyovitaka kwa familia yako




- Jaribu kufikiria orodha ambazo sio vitu kama vile vitu vya kushukuru' au 'vitu unavyofurahia kuvifanya'.
- Chagua jambo moja na uandike orodha yake.
- Je! Unaweza kugawanya orodha hiyo katika orodha ndogo ndogo? Kwa mfano, mimea kwenye eneo lako inaweza kugawanywa katika mambo ambayo unaweza kula na mambo ambayo huwezi kula.


**Umri:** Wowote
**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo
**Utakachojifunza:** Makuzi ya lugha; kuandika; tahajia
**Utakachokifanya:** Kupanga, kupangilia, ubunifu

# Tengeneza ramani ya eneo lako

**Utahitaji:** Penseli au kalamau na karatasi, viungo vya kupikia na vyombo vya kupikia

## Mambo ya kufanya:

- Chukuwa karatasi na penseli, kimsingi ni rangi chache tofauti.
- Fikiria kama unafanya matembezi ya kuzunguka eneo lako. Unaona nini? (Nyumba, majengo na barabara lakini pia miti au sehemu maalumu kama makanisa, misikiti au maeneo za kucheza).
- Fikiria juu ya mitaa ina ukubwa gani, miti au majengo yna urefu gani. Je! kuhusu sehemu za wazi kama shamba au pori? sehemu ya Soko? Shule? kuna vitu vyovyote vile unaweza kuvifikiria?




- Amua jinsi utakavyochora ramani yako. Je! Utapaka rangi katika vitu tofauti? Je! Utabuni ufunguo wa kuwakilisha vitu vyengine (kama mstari wa upinde unaoonesha mkondo, duara la kijani kwa mti,) au yachore yote?
- Je! Karatasi yako itahitaji kuwa na kubwa gani? Karatasi moja? au Mbili?
- Je! Kila kitu kitapaswa kuwa na ukubwa au udogo gani? Kama skuli, sehemu ya kuchezea, mitaa au njia? Soko?

- Chora ramani. Weka alama maeneo tofauti au tengeneza ufunguo na uweke alama hiyo.

**Muendelezo wa zoezi:**

- **Fikiria:** mtu mgeni anakuuliza mielekeo ya kwenda katika soko au mtoni. Andika au mueleze namna atakavyoweza kufika huko. Tafuta mtu wa kuangalia ramani yako na kuuliza mielekeo ya sehemu mbalimbali.

- **Simulia / andika hadithi** juu ya sehemu fulani katika eneo hilo (Je! skuli ilianza lini? Je! Kulikuwa na nafasi ya kawaida ya kuchezea? Jee! Kulikuwa na janga kama mafuriko au upepo mkali uliowahi kutokea katika eneo hilo? Kuhusu sherehe? jee kuna historia yoyote muhimu? Je! Kuna hadithi ya mambo ya kiroho kuzungumzia katika sehemu hiyo?

- **Tengeneza mfano** wa eneo hilo. Tumia vifungashio maboksi madogomadogo ya zamani unayoweza kuyapata. Je! Unaweza kuvitengeneza ili mtu asieona aweze kuhisi na kupita? kamba inaweza kukusaidia pia.

**Umri:** Wowote

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Wastani / high

**Utakachojifunza:** Ukuzaji wa lugha; msamiati wa maeneo; lugha kwa maelekezo; eneo la ndani, alama muhimu

**Utakachokifanya:** Ubunifu, uratibu, kuchora kwa kiwango, uwakilishi, kuelewa, uchunguzi

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:**

- Elezea eneo hilo na muombe mtu akusaidie kuchora ramani
- engeneza mfano (badala ya ramani) ya eneo hilo,
- Panga sehemu za nyumba yako au chumba kimoja ndani ya nyumba
- Simulia hadithi juu ya mahali unapoishi na muombe mtu aandike

# Tengeneza mtoto bandia kwa soksi

**Utahitaji:** Soksi ya zamani, safi, ndefu, kalamu nene au chaki, Vifungo vya zamani, Sindano, uzi, mkasi na pamba

## Mambo ya kufanya:

- Tafuta soksi ndefu ya zamani. Tia mkono wako ndani yake na ufanye umbo la C pamoja na vidole vyako na kidole gumba. Ingiza kidole gumba chako kwenye kisigino cha soksi. Cheza cheza nayo mpaka ionekane kama kichwa na mdomo.
- Tumia kalamu au chaki kuashiria sehemu ya macho yatakapokuwa. Itoe soksi. Chora macho mawili au shonea vifungo viwili ambapo uliweka alama ya macho.
- Ongeza pamba kutengeneza nywele. Ili kufanya hivyo kata vipande vya pamba vyenye urefu sawa na uzifunge katikati. Kisha zishonee kwenye soksI, juu ya macho.
- Mpambe mtoto wako wa bandia. mvalishe kofia ndogo au mfanyie mdomo kwa kutumia kadi au kitambaa
- Mpe mtoto wako wa bandia jina na fanya mazoezi kwa kumfanya mtoto wako wa bandia aseme. Mfanye apendeze ili achekeshe au wa kusikitisha kwa namna unavyochezesha mkono wako. Mfanye awe wa kushangaza kwa kuleta macho yake pembeni au kukasirika kwa kuleta macho yake karibu.

## Muendelezo wa zoezi:

- Tengeneza mtoto mwengine wa bandia kwa kutumia soksi na uwafanye wawe wanazungumza . Nini haiba/sifa zao? Je! Wana matukio gani? Waoneshe familia yako mtoto wa bandia wa soksi.



**Umri:** Msingi

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Wastani

**Utakachojifunza:** Kuchora, mazungumzo, ukuzaji wa lugha

**Utakachokifanya:** Uratibu, ubunifu, ufaraguzi

# Bao au mithili ya mchezo huo

**Utahitaji:** Penseli au kalamu na karatasi

**Mambo ya kufanya:**

- Michezo gani ya kuhesabu iliopo katika nchi yako? Mna michezo yoyote mnayocheza kwa kutumia changarawe, mbegu kavu za nafaka au vitu vyengine vya kuhesabia pamoja na bao (mithili ya lililooneshwa hapa chini)?

- Mnachezaje mchezo huo? Unazijua kanuni za mchezo? Kama huzijui, unaweza kumtafuta mtu wa kukufunza?

- Kama huna 'bao' unaweza kuchimba mfano wake kwenye ardhi? Unaweza kuchimba vishimo vidogo vidogo kwenye ardhi na kutafuta changarawe kwa ajili ya kuchezea.

- Cheza. Ukihitaji mcheze wawili itakupasa kumtafuta mwenza wa kucheza nae. Jambo gani linaufanya mchezo huu uvutie? Unaimarisha aina gani ya ujuzi?





### Muendelezo wa zoezi:

- Je! unaweza kuandika maelekezo ya jinsi ya kucheza mchezo unaoupenda? Chukulia kwamba maelekezo hayo ni kwa ajili ya mtu ambaye hajawahi kucheza mchezo huo hapo kabla.
- Unaweza kubuni aina nyengine ya mchezo wa kuhesabu? Mfundishe jirani yako. Je! Mchezo huo una kanuni zipi?

**Umri:** Wowote

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Kuhesabu, kukuza lugha (kutoa maelekezo)

**Utakachokifanya:** Ushirikiano, utatuzi wa shida, mawasiliano, mikakati

# Kutazama mazingira

**Utahitaji:** Penseli au kalamu na karatasi

## Mambo ya kufanya:

- Nenda nje na chagua kitu ambacho ungependa kukiangalia. Labda ungependa kuangalia wadudu kama vile buibui akijenga nyumba yake au sisimizi akichukua chakula. Inawezekana pia ungependa kutazama mdudu anayeruka kama vile kipepeo, ndege au nyuki akikusanya mbegu katika maua. Au ungeangalia miti na vivuli vyake vinavyoyumbayumba huku upepo ukivuma au mwangaza wa jua unavyoakisi kwenye mto.

- Tazama angalau kwa robo saa au zaidi na nukuu kila utachoweza kukinukuu. Angalia jinsi anavyotembea, na iwapo ana alama au rangi maalumu, (rangi zilizokoza zinazoashiria uwepo wake au rangi zinazomfanya asionekane kwa urahisi). Je! unaweza kumuelezea?

- Jiulize maswali mengine: Ana ukubwa gani? Ana miguu mingapi? Anatembeaje? (haraka haraka, taratibu, vibaya, anafurahisha). Anakwenda wapi? Kuna vizuizi gani katika njia anayopita, anafanya nini au anajaribu kutengeneza nini? Je! Kuna wadudu wengine/ wanyama wanaofanana na yeye karibu yake? Wanafanya nini?





**Muendelezo wa zoezi:**

- **Chora** picha ya ulichokiona.
- **Dadisi** zaidi kuhusu ulichokiona. Muulize mtu mwenye elimu ya vitu hivi baada ya kutafakari maswali ya kumuuliza. Je! Mnyama/mdudu huyu anakula nini? Wapo wa aina ngapi? Anatafutaje chakula chake? Je! Wanaishi katika vikundi au wakiwa mmoja mmoja? Wanazaliana vipi? Je! Wana tabia ya kuhamahama?
- **Tengeneza kitabu cha mazingira.** Hii inaweza kuwa ni karatasi ambayo utaandika au kuchora vile unavyoviona kila siku. Iwapo utaangalia kitu hicho hicho kwa siku kadhaa (mfano vivuli vya miti au mauwa yaliyochanua au mto, angalia mabadiliko yanayojitokeza kila siku). Je! Kuna wadudu wa aina tofauti wanaotua kwenye mauwa? Unauonaje mti? Je! Ndege wanautembelea mara kwa mara au majani yanabadilika? Je! inakua? Vipi kuhusu mto? Je! una samaki au wadudu waliomo ndani au wanaouzunguka? Je! Rangi ya maji inabadilika?



**Umri:** Wowote

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Kukuza lugha, uwezo wa kuelezea, sayansi: elimu ya mazingira na viumbe hai.

**Utakachokifanya:** Uwezo wa kutafiti kwa umakini na ukaribu. Kujifunza kupitia ulichokiona. Uvumilivu, kufikiri kwa umakini, mawasiliano.

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:** Iwapo huoni vizuri, tumia hisia zako nyengine (si kuona pekee) ili kutambua mazingira yanayokuzunguka. Sikiliza, nusa na gusa ardhi, miti na mimea inayokuzunguka. Elezea harufu ulioihisi, au ulichosikia na kuhisi kwa kugusa. Msimulie mtu mwengine ili aweze kunakili/kuandika.

# Wimbo mpya, sauti/mahadhi ya kale

**Utahitaji:** Hapana

**Mambo ya kufanya:**

- Fikiria nyimbo ambayo watu wote wanaijua na ni rahisi kuiimba
- Buni maneno mapya ukitumia sauti ya zamani. Unaweza kubuni nyimbo kuhusu chochote unachotaka, kwa mfano, jinsi ya kusafisha meno, muhusika wa simulizi unayoipenda, au jambo la kuchekesha lililowahi kukutokea.
- Wafundishe wengine jinsi ya kuiimba nyimbo hiyo. Ukipenda ongeza na vionjo vyengine.
- Huu hapa ni mfano wa nyimbo ya 'kuosha mikono' ikiwa na sauti ya nyimbo ya 'Alfoola Alfoola'. Je! Unaweza kuiimba nyimbo hiyo?

Osha mikono yako, Osha mikono yako
Kwa nini, Kwa nini?
Osha ondoa vijiduudu
Sugua sugua, futa iwe safi

Ondoa vijiduudu
Osha mikono yako, mbele na nyuma
Osha vidole vyako pia kucha
Vijiduudu vitakimbia.



**Umri:** Msingi

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** makuzi ya lugha, mapigo, silabi, istilahi za kishairi

**Utakachokifanya:** Ubadilishaji, ubunifu/ utunzi

# Shairi lisilo na maana

**Utahitaji:** Kalamu/penseli na karatasi

## Mambo ya kufanya:

- Litazame shairi 'lisilo na maana' lililotungwa na Spike Milligan. YUkipenda unaweza kulisoma kimya kimya au kwa sauti. Kuwa makini kugundua neno lolote la kuchekesha au lisilotarajiwa.

**Kwenye Ning Nang Nong**


Kwenye Ning Nang Nong
Ambapo ng'ombe hulia Bong!
na kima wakisema BOO!
Kuna Nong Nang Ning
Ambapo miti hulia Ping!
Na birika za chai jibber jabber joo.
Kwenye Nong Ning Nang
Panya wote hulia Clang
Na huwezi kuwashika wanapofanya hivyo!
Kwa hivyo Ning Nang Nong
Ngo'mbe hulia Bong!
Nong Nang Ning
Miti hulia Ping
Ning Ning Nang
Panya hulia Clang
Ni sehemu yenye kelele nyingi kwa mtu kuishi
Ni Ning Nang Ning Nang Nong!!

**On The Ning Nang Nong**

On the Ning Nang Nong
Where the Cows go Bong!
and the monkeys all say BOO!
There's a Nong Nang Ning
Where the trees go Ping!
And the tea pots jibber jabber joo.
On the Nong Ning Nang
All the mice go Clang
And you just can't catch 'em when they do!
So its Ning Nang Nong
Cows go Bong!
Nong Nang Ning
Trees go Ping
Nong Ning Nang
The mice go Clang
What a noisy place to belong

- Baada ya kumaliza kusoma, andika orodha ya maneno yote yasio na maana ambayo Spike Milligan aliyatumia katika shairi hili.
- Ni neno lipi lisilo na maana ulilolipenda zaidi na kwa nini?
- Je! Mna mashairi yoyote ya kuchekesha katika nchi yenu/lugha?
- Andika maelezo (maana) ya maneno yaliopo hapo juu ambayo yatawapumbaza (kitendawili) rafiki zako.
- Jaza mapengo kwa kutumia maneno uliyoyabuni kuelezea vitendo au sauti:
  - Upepo ............................................ kwenye miti.
  - Sauti ya kucha ubaoni: ............................................
  - ............................................: kitendo cha kinyesi cha ndege kudondoka njiani

- Vumbua maneno yako mwenyewe na maana zake.
- Sasa andika shairi lako **lisilo na maana** ukitumia baadhi ya maneno yako yasio na maana.
- Chagua yale unayoyapenda ambayo ukiyaweka pamoja yanapendeza zaidi.
- Unaweza kutumia shairi la 'Kwenye Ning Nang Nong' kama mfano. Jaribu kutunga shairi lako ukianza na maneno, kama vile:
  - Kwenye ...
  - Ambapo ...
  - Na ...
  - Yote ...










**Umri:** 8+

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Kukuza lugha, maana, muundo wa sentensi, beti na mapigo

**Utakachokifanya:** Ubunifu, mawasiliano, kubuni maana

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:**

- Tunga shairi lako kwa kuimba au muombe mtu mwengine akuandikie.
- Andika shairi la mistari miwili miwili.

# otesha mmea na shuhudia ukikua

**Utahitaji:** Mbegu, udongo, maji, kipima kimo

## Mambo ya kufanya:

- Chagua mmea utaoamua kuuotesha. Kunde, fiwi, mbegu nyengine? Unataka kuotesha mmea wa chakula? Chunguza ni mbegu gani hustawi vyema katika msimu huu na mbegu zipi zinapatikana.
- Amua utaotesha wapi mbegu hiyo. Kwenye kopo la kuoteshea au chini ya ardhi. Na kama ni kwenye ardhi, chagua mahali ambapo hakuna uwezekano wa kuharibiwa na wanyama. Chunguza sehemu ilio bora kwa ajili ya kuoteshea. Mahali palipohifadhiwa? Pakiwa na kivuli au mwangaza hafifu wa jua?
- Otesha mbegu yako katika eneo ambalo halina magugu. Otesha mbegu mbili au tatu za aina moja katika kopo moja kwa ajili ya tahadhari iwapo nyengine haitomea. Tilia maji.
- Tengeneza lebo kwa ajili ya mmea wako. Andika jina la mmea kwenye kijiti na kichomeke kwenye udongo karibu na hiyo mbegu.
- Tilia maji kila siku au kadiri inavyotosheleza ili kuufanya udongo uwe na unyevu.

## Muendelezo wa zoezi:

- Kila siku chunguza/fuatilia ukuaji wake. Weka rekodi ya ukuaji. Pima kimo cha mmea kila siku kuanzia siku ulipochipua. Imechukua siku ngapi kuota majani? Mauwa? Tunda? Andika ulichokiona.



**Umri:** Wowote

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Kuotesha mmea wa chakula, mazingira ya asili, jinsi ya kuuhudumia mmea

**Utakachokifanya:** Utafiti, utatuzi wa shida

# Kusoma pamoja

**Utahitaji:** Kitabu cha hadithi/simulizi

## Mambo ya kufanya:

- Kaka/dada anaweza kumsomea hadithi ndugu yake, au ndugu anaweza kumsomea kaka au dada yake au mzazi wake. Wakati mwengine ni vyema kusomeana kwa zamu.
- Chagueni hadithi (kutoka kwenye kitabu) ambayo nyote wawili mnaipenda au tafuteni hadithi mpya. Inaweza kuwa ni hadithi ya kweli au ya kubuni tu.
- Kumbuka kusoma kwa hisia. Utaigizaje sauti ya simba, ajuza (kikongwe), sungura mwenye hofu?
- Uwe unasita wakati ukiendelea kuhadithia na kuuliza 'unadhani kitatokea nini?'. Jaribuni nyote kwa pamoja kutabiri kitachotokea katika sehemu ijayo ya simulizi.
- Katika ukurasa ufuatao kuna hadithi nyengine ambayo mnaweza kuisoma pamoja. Soma sehemu kuu ya simulizi, halafu sita kabla hujamaliza na jaribu kutabiri itamalizikaje.
- Malizia sehemu iliobaki. Je! Ulipatia? Unaweza kubuni jina kwa ajili ya hadithi hiyo?
- Je! Mnaweza kuigiza kwa pamoja, moja kati ya hadithi mnazozipenda? Amua ungependa uwe muhusika gani na fanyia mazoezi kipengele hicho. Igizeni simulizi hiyo mbele ya wanafamilia wengine.

**Muendelezo wa zoezi:** Je, mnaweza kuigiza moja ya hadithi unazozipenda sana? Amua ni wahusika gani utakao kuwa nao na ufanyie mazoezi igizo lako . Simulia hadithi yako kwa wanafamilia wengine.

**Hadithi ya 1: Tembo:**

'Usiende mtoni' mama tembo aliendelea kusisitiza kwa kumwambia mwanawe. 'Kuna mamba mkubwa huko, atakumeza.' Mtoto wa Tembo akitamani kujua. Mamba ni kitu gani? Lakini hakuna yeyote alieyempa jawabu. Kwa hivyo, alienda kwenye mto. Alisimama karibu na kingo ya mto. Kisha akasogea karibu kidogo. Lakini hakuweza kuona kitu isipokuwa uso wake mwenyewe tu katika mto. Alisogea karibu zaidi na ghafla ... mamba akatokea na kutanua taya zake na kumnyakua mtoto wa tembo! ...

Alimbana Tembo kwa pua. 'Nisaidieni' alipiga kelele Tembo. Mama yake akaja mbio, akaushika mkia wake. Kaka zake walikuja mbio na walimshika masikio yake, na walijitahidi kumvuta lakini mamba hakumwachia. 'Tusaidieni' walisema kwa sauti kubwa na mara kila mmoja kwenye msitu alikuwa akimvuta mtoto wa tembo.

**Mwisho:**

Waliuvuta mkia wake na ukawa mrefu kama kamba, walivuta masikio yake na yakakua na kuwa makubwa, na pua yake ilikua ndefu, ndefu sana. Wakaendelea kuvuta hadi mamba alipomwachia. Kila mmoja alianguka juu ya mwengine kwenye nyasi. Mtoto waTembo alikuwa salama. Lakini ni nini kilikuwa kimetokea kwa mkia wake mdogo uliokuwa umejaa na masikio yake madogo, na ..... PUA yake? Ndio maana hadi hivi leo, tembo wana pua refu zinazoitwa mikonge na masikio makubwa kama majani ya kabichi.

## Hadithi ya 2: Matone matatu ya mvua (na Terry Jones):

Tone moja la mvua lilikuwa likinyesha kutoka mawinguni, na likamwambia tone la mvua lililokuwa kando yake: 'Mimi ndiye mvua kubwa na bora angani kwote! 'Kwa kweli wewe ni tone dogo tu la mvua,' akasema wa pili, 'lakini umbo lako sio zuri sana kama mimi. Na kwa maoni yangu, umbo, ndio muhimu kuliko mambo yote na kwa hivyo mimi ndiye tone bora zaidi la mvua angani. 'Tone la kwanza likajibu: 'Wacha tulitatue suala hili mara moja.' Kwa hivyo, waliliomba tone la tatu kuamua kati yao. Lakini tone la tatu lilisema: 'Mnaongea upuuzi gani! Unaweza kuwa tone kubwa, na hakika ukawa umeumbwa vizuri, lakini, kama kila mmoja ajuavyo, usafi ndio muhimu zaidi, na mimi ni safi kuliko nyote nyie wawili. Kwa hivyo mimi ndiye tone bora zaidi angani!

**Mwisho:**

Kabla ya yoyote kati ya matone mengine hayajajibu, matone yote matatu yakaanguka ardhini na kuwa sehemu ya dimbwi lenye matope mengi.

**Umri:** Wowote

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** High

**Utakachojifunza:** Kukuza umahiri wa lugha/ muundo wa simulizi, utabiri, igizo

**Utakachokifanya:** Ubunifu, kusaidiana, ushirikiano, kusikiliza

# Msaka vilivyotupwa

**Utahitaji:** Karatasi na penseli

**Mambo ya kufanya:**

- Kusaka vilivyotupwa ni pale unapotakiwa kwenda kutafuta vitu ulivyopewa kwenye orodha. Unaweza kusaka 'ndani' au nje. Ukisaka na wengine, ataekuwa wa mwanzo kuvipata vyote vilivyoorodheshwa ndiye mshindi.
- Angalia orodha. Ukiwa peke yako au ukishirikiana na wengine, kwa muda gani utavikusanya vyote vilivyomo kwenye orodha?

  - Something soft/ Kitu laini
  - Vitu viwili vilivyotengenezwa kwa mbao
  - Kitu kitamu
  - Vitu vitatu vinavyoanza na P
  - Kitu kinachong'ara
  - Kitu kinachotumika kufanyia usafi
  - Kitu unachokipenda

- Iwapo utakua unashirikiana na mwengine, linganisheni vitu tofauti mlivyovikusanya.
- Sasa tengeneza orodha yako. Utakua umeanza vizuri iwapo utatumia maneno (laini, tamu, inang'ara) na rangi. Angalia mifano myengine iliopo hapo juu na fikiria iwapo unaweza kutengeneza orodha yako mwenyewe ya vitu 10 kwa ajili ya kuvitafuta
- Andika orodha yako ya vitu na muombe mwenzako akavitafute.



**Umri:** Wowote

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Kukuza umahiri wa lugha (vivumishi na nomino), kuhesabu

**Utakachokifanya:** Ubunifu, utatuzi wa shida, ushirikiano

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:**

- Chagua vitu vilivyomo katika chumba kimoja tu nyumbani kwenu.
- Ashiria na muombe mwenzako akuletee.
- Mtajie (mwenzako) sifa za hivyo vitu na mtake akuandikie hiyo orodha.

# Fumbo


**Utahitaji:** Karatasi na penseli

## Mambo ya kufanya:


Kuna namna nyingi za kuandika fumbo lako la siri.

- Unaweza kuziwakilisha herufi katika alfabeti zako kwa kutumia nambari lakini anza na nambari kubwa na uziorodheshe kutoka kubwa kuja ndogo. Kwa mfano, Kiingereza kina herufi 26, kwa hivyo a=26, b=25, c=24, d=23 n.k. Je! Unaweza kufumbua fumbo lifuatalo?
  8 22 24 9 22 7   24 12 23 22

- Unaweza kuiwakilisha herufi moja kwa kutumia herufi nyengine katika alphabet lakini ziweke kwa mpangilio, kwa mfano a=h, b=I, c=j, d=k, e=l, f=m n.k.



- Unaweza pia kubuni alama mpya kuwakilisha kila herufi ya alfabeti kama unavyoona kwenye mfano. Iwapo umeamua kubuni alama zako mwenyewe, jiulize:
  - Nambari zangu za siri zianzie kushoto kwenda kulia? Au zianze juu kuja chini?
  - Je! Niwe na idadi sawa ya alama kama idadi ya herufi za alfabeti? Au alama mbili ambazo zitawakilisha herufi moja? (Hii inafanya iwe vigumu kwa wengine kugundua).
- Unaweza kubuni maneno ya Kiswahili kwa kutumia alama ulizopewa hapo juu? (Kumbuka, hujapewa alama zote!)



- Weka kalamu/penseli na karatasi yako tayari. Andika fumbo lako kwa

**Umri:** Wowote

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Makuzi ya lugha, kuandika, herufi

**Utakachokifanya:** Ubunifu, mawasiliano, kutatua shida

# Maumbo na nakshi katika mazingira yetu

**Utahitaji:** Vijiti na mawe

## Mambo ya kufanya:

- Toka nje ya nyumba yenu. Angalia kuna aina ngapi za maumbo tofauti na nakshi ambazo unaziona katika mazingira ya asili? Pia angalia vitu ambavyo vimetokana na mazingira ya asili vilivyomo nyumbani kwenu, kama vile matunda na mboga mboga.



- Ni maumbo na nakshi ngapi unazoweza kuzitaja? Je! Unaweza kutafuta kitu ambacho:
  - Kinalingana?
  - Chenye umbo la mawimbi?
  - Duwara au mviringo?
  - Nakshi zake zinajirudia rudia?
  - Kina umbo la nyota au kopa?

- Umeona baadhi ya majani ambayo yanaonekana kama ni mti kamili lakini mdogo? Umeliona jani kama hili? Unaweza kuhesabu idadi ya sehemu ndogo ndogo kwenye mgongo wa jani?

- Kusanya vijiti na mawe. Ni maumbo gani mengine ambayo unaweza kutengeneza kwa kutumia vitu hivi?
  Unaweza kutengeneza:
  - Pembe tatu au mraba
  - Umbo la pembe tano
  - Umbo la pembe sita
  - Umbo la pembe nane



- Je! Unaweza kutengeneza umbo lolote lenye muonekano wa pande tatu kwa kutumia vijiti na mawe? Piramidi au umbo la bomba?

**Umri:** Wowote

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Majina ya maumbo, majina ya nakshi, kuhesabu

**Utakachokifanya:** Ubunifu, utatuzi wa shida, uratibu, uchunguzi

# Mzunguko wa hadithi

**Utahitaji:** Penseli au kalamu na karatasi

**Mambo ya kufanya:**

Unaweza kufanya zoezi hili ukishirikiana na watu watatu au zaidi. / Kaeni pamoja kwenye duara.

- Mmoja ataanza kusimulia, kwa mfano, "Alikuwepo binti mdogo ambaye alikuwa hapati usingizi. Aligaragara kitandani lakini hakuupata usingizi".
- Sita hapa. Muombe mwengine aendelee na hadithi kwa kusimulia sentensi moja au mbili, kwa mfano,:

  "Aliendelea kuuangalia mwezi mkubwa wenye umbo la duara. Ghafla kikatoka kitu kutoka kwenye mwezi kikimuelekea yeye. Ilikuwa ni ngazi ya rangi ya fedha ambayo ilishuka chini, chini,chini, mpaka usawa wa dirisha lao".
- Muachie mtu mwengine wa tatu aendelee au mrudie wa mwanzo iwapo kuna wasimuliaji wawili pekee. Kwa muda gani utaiacha hadithi iendelee?
- Muombe mmoja wenu aimalizie baada ya kwamba nyote mmepata kusimulia angalau mara mbili
- Kanuni za 'Mzunguko wa hadithi' ni:
  - Tumia ubunifu wako!
  - Iendeleze hadithi (huwezi kusema, 'alipanda ngazi' halafu ukasita hapo, inakubidi uendeleze zaidi 'alipanda ngazi mpaka alipofika juu akaona ………')
  - Usisimulie hadithi yote, mpe nafasi mwengine aendeleze.

- Unaweza kuchagua aina yoyote ya hadithi. Inaweza kuwa inahusu kitu cha kweli (kama vile sherehe au safari) au mnyama au simulizi ya kubuni kutoka mawazoni



**Umri:** Msingi

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Kukua kwa umahiri wa lugha, muundo wa simulizi na kanuni za kutunga hadithi.

**Utakachokifanya:** Uwezo wa kufikiri kwa haraka, ubunifu, mawasiliano na ushirikiano

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:**

- Chukua vitu vidogo vidogo 10 ulivyoviokota karibu na nyumba yenu na uviweke kwenye kapu - chochote kile kilichopo, (kwa mfano kikombe, jiwe, kitambaa...); toa kitu kimoja kimoja kutoka kwenye kapu, kila utapotoa kitu kingine kitumie kutunga na kuongeza sentensi moja au mbili kwa ajili ya hadithi yako. Kwa mfano, 'alipofika juu ya ngazi aliona kikombe, kilikua kikombe cha dhahabu na kilikua kimejaa na kudondosha kimiminika cha ajabu cha rangi ya dhahabu.....'
- Iandikeni simulizi yenu nzuri mlioitunga pamoja. Iongeezeni vivumishi na vielezi ili kuifanya ivutie zaidi.

# Kumshukuru shujaa wa kijiji

**Utahitaji:** Karatasi na penseli

## Mambo ya kufanya:

- Shujaa wa kijiji anaweza kua ni mtu yeyote wa kawaida ambaye anawasaidia wengine hapo kijijini au alikuwa jasiri kwa kutokata tamaa licha ya kukutana na changamoto nyingi. Yeyote anaweza kuwa shujaa. Je! Unamfahamu yeyote mwenye sifa hizi?

- Fikiria kuhusu shujaa wa kijijini kwenu. Ni akina nani hao? Walifanya nini? Nini unawahusudu?

- Ungependa kumshukuru vipi shujaa wenu? Kuchora mchoro wa picha yake, kubandika bango lenye picha yake au kutunga wimbo wa kusherehekea mafanikio yake? / Kumuandikia barua ya shukurani au kumpatia aina nyengine za zawadi? Au labda kumwambia tu 'Ahsante".



- Andaa zawadi yako/ andika barua halafu tafuta namna nzuri ya 'kuiwasilisha' kwa shujaa wako. Muombe mzazi wako au kaka/dada yako kukusaidia katika hili.

**Umri:** Msingi

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Kukuza lugha

**Utakachokifanya:** Mawasiliano, ubunifu, kuonesha upendo na kuguswa

# Kusaka Hazina

**Utahitaji:** Penseli au kalamu na karatasi

## Mambo ya kufanya:

Kusaka hazina ni mchezo ambao wachezaji hutafuta kitu kilichofichwa kwa **kufuata viashiria/vidokezo** Kila kiashiria utakachokifuata kitakusogeza kwenye kiashiria chengine mpaka utaipata mali iliyofichwa. Mwisho 'mali' inaweza kuwa chochote kile unachokitaka – kitu kidogo cha kufurahisha/kuvutia au chakula (muhimu uhakikishe kwamba hapo kitapofichwa hakigunduliwi na mnyama asije akakila kabla hujakipata!)

- Fikiria **nani unataka ucheze nae mchezo huu** – ndugu yako au kaka/dada yako? Mtu mzima? Itakupasa ubuni viashiria vinavyolingana na umri wao ambavyo watavifahamu kwa urahisi (angalia baadhi ya mifano hapa chini).

- Chagua **sehemu** (sehemu ambazo alama zitawekwa) **kwa ajili ya kusaka hazina**. Mti mkubwa, kabati lililopo nyumbani, au alama inaweza kuwa mwanafamilia mwengine ambae hashiriki katika mchezo. Kiasi cha maeneo 8 yanatosha. Yaandike hayo maeneo na yaorodheshe kwa mpangilio maalumu.

- **Andika kiashiria cha kila eneo katika vikaratasi tofauti.** Hakikisha kwamba viashiria hivi vinafahamika na 'washiriki wa mchezo' lakini usivifanye vikawa rahisi mno! Kwa mfano:

  - Kiashiria: Nina tunda tamu la rangi ya chungwa, linalonata (Eneo: Muembe)

  - Kiashiria: Hapa ndipo unapoota njozi usiku (Eneo: kitandani)

  - Alama: TREWA NICEROTAN (Eneo: Water Container)

- **Vipe nambari vile viashiria** na uvikunje huku nambari pekee ikiwa ndio yenye kuonekana. Utawapa washiriki wa mchezo kiashiria cha mwanzo ambacho kitawaongoza kuelekea kwenye kiashiria chengine

- **Chukua kiashiria cha mwanzo na kihifadhi, na ficha vilivyosalia** katika maeneo katika mpangilio sahihi – tumia orodha uliokaiandaa hapo kabla kukusaidia kukumbuka sehemu za kuficha. Kwenye kiashiria nambari 1 ndipo utapokificha kiashiria nambari 2. Kwenye kiashiria nambari 2 ndipo utapoficha kishiria nambari 3 n.k. Kwenye kiashiria cha mwisho ndipo utapoweka 'mali'.

- Iwapo kuna mshiriki zaidi ya mmoja, kubalianeni juu ya kanuni za mchezo pamoja. Kanuni inawezakuwa kwa mfano:

  - Tunapaswa kusubiriana kabla ya kwenda kwenye kiashiria chengine.

- **Kabidhi kiashiria cha kwanza.** Ongozana nao washiriki iwapo watakwama na wakahitaji msaada ili watambue viashiria.

**Umri:** 10+

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Wastani

**Utakachojifunza:** Kukuza lugha; kuandika, tahajia

**Utakachokifanya:** Kupanga, mtiririko, ubunifu, kufikiria kwa umakini, mawasiliano, ushrikiano, utatuzi wa shida

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:**

- Muombe mtu mwengine akusaidie kuandika viashiria.
- Andika viashiria vitatu tu au vinne.
- Usifanye mchezo wa kusaka hazina kama 'jaribio' bali kila kiashiria kinakuongoza katika 'mali' – hii inakua rahisi kupangilia.

# Maswali Ishirini

**Utahitaji:** Hapana

## Mambo ya kufanya:

Mchezo huu unapendeza zaidi wakishiriki kati ya watu wawili mpaka watano ili kila mmoja apate kuuliza swali.

- Unaweza kumchagua yeyote aanze katika kikundi chenu. Kwa mfano, yule aliye mdogo kuliko wote au ambaye sherehe ya siku yake ya kuzaliwa ilikua hivi karibuni.

- **Chagua mtu, mahali, au kitu.** Mfikirie mtu ambaye unamjua vya kutosha ambae utaweza kujibu maswali kumuhusu yeye. Iwapo utaamua mtu, basi anaweza kuwa aliye hai au aliyekwishafariki, au hata wa kufikiria tu (kutoka katika simulizi fulani). Hakikisha unamchagua mtu, mahali, au kitu ambacho wengi katika kikundi chako wanakijua.

- Washiriki wengine watauliza maswali ya ndio au hapana. Anza na swali la jumla swali la 'wazi' ambalo linaweza kujibiwa kwa "ndio" au "hapana". Kwa mfano:


    - "Je! Ni mtu?"
    - "Je! Ni mahali?"
    - Je! Ni kitu?
    - "Ni kitu cha kweli au cha kufikirika?"

- Ulizaneni kwa zamu maswali ya ndio au hapana. Hakikisha kila mshiriki anapata nafasi ya kuuliza angalau swali 1. Iwapo mshiriki atauliza swali ambalo haliwezi kujibiwa kwa "ndio" au "hapana", muombeni alitunge upya ili liweze kujibiwa kwa namna hiyo. Kwa mfano, mshiriki asiulize, "wana umri gani?" lakini aulize, "Je! Wana umri zaidi ya miaka 50?"

- Uliza maswali makhususi zaidi kadiri mchezo unavyoendelea. Kumbuka maswali yaliyoulizwa, kabla hujauliza maswali mapya. Kwa mfano, iwapo kuna aliyeuliza kuhusu kiwango cha ukubwa, endelea kwa kuuliza kuhusu rangi au malighafi iliotengenezewa kitu.

- Chezeni mpaka mfike maswali 20 au mshiriki atapotoa jibu sahihi. Hesabuni maswali pamoja. Iwapo kikundi kitakamilisha maswali 20 na wakashindwa kumtambua mtu, mahali, au kitu kilichokusudiwa, wape jibu sahihi. Iwapo mmoja wa washiriki atatoa jibu sahihi kabla ya kutimia maswali 20, mchezo utaishia hapo.

- Mfanye aliyepatia jawabu kuwa ndio muongozaji. Iwapo hakuna yeyote aliepatia jawabu kuhusu mtu, mahali, au kitu, yeyote atakayetaka anaweza kuendelea. Toa fursa kwa kila mtu kufikiria kitu fulani. Kumpa kila mmoja fursa kunaufanya mchezo uwe jumuishi zaidi na kumfanya kila mmoja afurahie.



**Umri:** Wowote

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Kukuza lugha; aina za vitu

**Utakachokifanya:** Mawasiliano, kufikiri kwa udadisi, utatuzi wa shida

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:**


- Weka ukomo wa maswali kwa kuchagua aina fulani ya vitu, m.f. 'wanyama', 'chakula' au 'watu mashuhuri'. Waambie washiriki ni kitu cha aina gani
- Chezeni katika timu za watu wawili wawili ili muweze kusaidiana katika timu yenu.
- Endeleza mchezo kwa kuongeza idadi ya maswali kupindukia 20 ili kuongeza nafasi ya kupata jibu sahihi.

# Barua kwa mwalimu wako

**Utahitaji:** Karatasi na penseli

## Mambo ya kufanya:

- Tayarisha penseli yako.
- Fikiria unachotaka kumueleza mwalimu wako. Je! Unataka kumueleza kuhusu unachofanya nyumbani? Unaweza kuandika:
    - Kitu kilichokufurahisha
    - Kitu cha kuchekesha kilichotokea
    - Jambo la kutumia akili ulilolifanya
    - Kitu fulani unachokitarajia
- Andika barua ikiwa na anuwani na tarehe, halafu weka saini yako.
- Ikiwezekana, unaweza kumpelekea mwalimu? Muombe mzazi wako au kaka/dada yako akusaidie.



Dear mrs roper,
I tryed Tee wicks and i loved it. It was funny when me and my mum got tangled up in the swing ball. I also tryed maths game, and all the different games on it. Some of them are difficult and some of them are really fun!. I'm looking forw-ard to making something out of wood. yours

sincerely

Theo:

**Muendelezo wa zoezi:**

- Unaweza kuandika jibu la 'kufikiria' ambalo mwalimu wako atakuandikia? Tumia aina ya maneno ambayo mwalimu wako unadhani atatumia

- Unaweza kumuandikia mwalimu wako barua ya kuchekesha ukimueleza kwa nini hukufanya kazi yako ya nyumbani? Fikiria udhuru 'usio wa kawaida', kwa mfano:

  - "mbuzi alikula kazi yangu ya nyumbani"
  - "upepo ulikua mkali mpaka ukapeperusha kazi yangu"

- Tumia mfano uliopo hapo juu ili ukusaidie kuandika barua yako.

Mwalimu mpendwa

Nisamehe kwa kutofanya kazi yangu ya nyumbani.

Nasikitika sana kwamba .... (kilichotokea)....

Nita...(utakachokifanya?)..........

Ahsante,

Saini:



**Umri:** Wowote

**Usaidizi wa mtu mzima/kaka/dada:** Mdogo

**Utakachojifunza:** Kukuza umahiri wa lugha, uandishi wa barua, muundo wa sentensi, herufi

**Utakachokifanya:** Ubunifu, kuguswa

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:**

- Msomee kwa imla mtu mwengine (unamuambia nae anakuandikia)
- Andika nukta muhimu
- Chora picha umuoneshe mwalimu wako vitu unavyofanya ukiwa nyumbani